



**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



## KIFUA KIKUU TANZANIA

Ugonjwa wa Kifua kikuu (TB) huandamana kwa karibu sana na ugonjwa wa UKIMWI na malaria na ni mojawapo ya magonjwa yanayosababisha vifo vingi nchini Tanzania, Tanzania ni kati ya nchi 30 zenye viwango vikubwa vya maambukizi ya Kifua kikuu na kifua kikuu / UKIMWI. Mkakati wa USAID dhidi ya kifua kikuu nchini Tanzania. unasaidia Mpango wa Taifa wa kupambana na Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) kushughulikia changamoto za kimfumo na kiutendaji kuzuia, kugundua, na kutibu ugonjwa huu. Hii ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma bora, inayozingatia wagonjwa wa Kifua kikuu, Kifua Kikuu / Ukimwi, na Kifua Kikuu sugu; kuzuia maambukizi na mwenendo wa ugonjwa; na kuimarisha majukwaa ya kifua Kikuu ya Tanzania kupunguza utegemezi wa ufadhili wa nje wa kifedha na kitaalamu. Mtazamo wa USAID nchini Tanzania unachangia kuboresha vipaumbele vya serikali, sekta binafsi, Shirika la Afya Duniani, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu, na Malaria, na mashirika mengine ya kimataifa kusaidia Mpango wa Taifa wa kupambana na Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP). USAID inatoa ufadhili huu kupitia mradi wake dhidi ya kifua kikuu, Challenge TB, mipango jumuishi ya utoaji wa huduma, na washirika wengine chini ya Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kupambana na UKIMWI. Katika Mwaka wa Fedha 2019, USAID / Tanzania ilisaini Mkataba wa Maelewano kati yake na Wizara ya Afya ya Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali za Mikoa na serikali za Mitaa kujitolea mpango wake wa Dunia wa kuongeza kasi na Kukomesha Kifua Kikuu. Mpango huu unaongeza rasilimali za umma na asasi zisizo za kiserikali na kujenga uwezo wa ndani wa huduma kwa mteja na wagonjwa wenye TB.

Katika mwaka wa fedha 2019 washirika wa USAID walifadhili shughuli zifuatazo:

- kuibua wagongwa wenye kifua Kikuu kwa kutumia zana bora za uchunguzi ikiwa ni pamoja na kugundua TB sugu
- Kuanzisha matibabu wagonjwa wenye kifua kikuu kwa kushirikiana na wahudumu wanaojitolea katika jammii, za Kifua Kikuu, asasi za kiraia, mashirika, na serikali za mitaa
- Kuanzisha dawa mpya na matibabu, pamoja na miongozo na mafunzo juu ya utumiaji mzuri, hususan TB

sugu

- Huduma jumisha za Kifua Kikuu na VVU katika mikoja iliopewa kipaumbele na kufanya kazi na vituo ili kuanzisha mifano ya kituo kimoja cha huduma katika eneo la matunzo na matibabu.

## **MUHTASARI WA KIFUA KIKUU**

### **KIWANGO CHA UFADHILI**

Dola za Marekani Milioni 5 Mwaka wa Fedha 2019

### **WASHIRIKA WAKUU**

- Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu
- Mfuko wa Dunia wa Kupambana Dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria
- Ufuatiliaji na Utambuzi wa Magonjwa ya Kuambukiza (IDDS)
- Sustaining Technical and Analytic Resources (STAR)
- Deloitte
- Elizabeth Glaser Pediatric AIDS Foundation
- John Snow, Inc.

### **ENEEO**

Nchi Nzima

### **MAWASILIANO**

Laurel Fain  
[lfain@usaid.gov](mailto:lfain@usaid.gov)

### **KWA MAWASILIANO ZAIDI**

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)

Facebook: USAIDTanzania

Twitter:  
@USAIDTanzania

## **CHANGAMOTO**

- Kuongezeka kwa uhaba wa wafanyakazi wa huduma ya afya kunaathiri mwendelezo na ubora wa uratibu wa kiwango cha wilaya na kituo, usimamizi, na ushauri dhidi ya Kifua Kikuu
- Haja ya kuboreshwa kwa huduma ya maambukizi ya TB na kinga hatua za kuthibiti maambukizi katika vituo vya afya na miongoni mwa wahudumu wa afya
- Utetezi usiotosheleza ili kuongeza uwekezaji wa ndani katika kuibua na tiba dhidi ya Kifua Kikuu

## **MATOKEO**

- Tumeka kwenye tiba dhidi ya Kifua Kikuu takriban wagonjwa 32,000 kutoka katika halmashauri 87 Mwaka wa Fedha 2019
- tumegatua huduma za TB sugu kote nchini, na kupunguza sana adha ya wagonjwa kusubiri muda mrefu kupata tiba
- Tumeongeza idadi ya maeneo yenye vifaa vya kudhibiti TB sugu katika maeneo 145 katika mikoja 26
- Tumeweza kuibua na kutoa taarifa ya wagonjwa wa kifua kikuu kwa asimia sita na kuibua na kutoa taarifa ya watoto wenye Kifua Kikuu kwa asilimia 15 katika mikoja inayofadhiliwa na USAID kwa kutoa vifaa bora vya uchunguzi, mafunzo ya Kifua Kikuu cha watoto, mipango ya uboreshaji, na kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi
- Tumedumisha kiwango cha mafanikio ya matibabu ya TB kwa asilimia 92
- Tumeisaidia NTLP katika kufuatilia utendaji wa programu na kuboresha usimamizi wa utekelezaji wa mradi wa TB
- Tuli fadhili kufanya uchunguzi wa sampuli zaidi ya 40,000 za makohozi na kuibua zaidi ya sampuli 1,541 zanye ugonjwa wa Kifua Kikuu kupitia APOPO (Anti-Personnel Landmines Detection Product Development.), shirika ambalo linafundisha panya buku kunusa na kuibua/kugundua vimelea vya TB kwenye makohozi.